

# MPYA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

WILAYA YA LINDI



## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI KATIKA MRADI WA MAJI RUTAMBA

Jumuiya ya Watumiaji Maji-RUTAMBA ni chombo huru cha kijamii cha watumiaji maji kilichoundwa kwa makubaliano ya wanachama/ Wanajumuiya wa Vijiji vya **Rutamba ya Sasa, Rutamba ya Zamani, Chilala na Michee** Kata ya Rutamba kama Jumuiya ya Watumiaji Maji. Jumuiya hii imeundwa na kusajiliwa kisheria kwa namba ya usajili **RUWASA/LINDI (W)/CBWSO/008** kwa mujibu wa kifungu cha 32 cha Sheria ya Huduma za Maji ngazi ya Jamii Na.5 ya mwaka 2019 na kanuni ya 3 ya Kanuni za Uundaji, Usajili na Uendeshaji wa Jumuiya.

### 1. MSIMAMIZI WA MRADI (NAFASI 1)

#### SIFA ZA MUOMBAJI

- (i) Awe na Cheti cha Kidato cha nne
- (ii) Awe na Cheti cha ufundi daraja la II na kuendelea
- (iii) Awe na uwezo wa kufanya kazi pamoja na kusimamia mafundi wasaidizi
- (iv) Awe na umri kuanzia miaka 18-35
- (v) Awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa
- (vi) Awe rala wa Tanzania
- (vii) Awe mwaminifu na mwadilifu na asiwe amewahi kufungwa jela

#### MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa Jumuiya ya Watumiaji Maji katika ngazi ya Jamii na Katibu wa Jumuiya ya Watumiaji Maji
- (ii) Kusimamia na kutekeleza shughuli zote za uendeshaji wa Mradi wa Maji
- (iii) Kusimamia ukusanyaji wa Ankara za Maji na kutunza nyaraka zote za shughuli za uendeshaji wa mradi
- (iv) Kuhakikisha huduma ya Maji yenye ubora inafika kwa wateja/ wananchi
- (v) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za mradi, Mfano:-Taarifa ya mapato na matumizi, taarifa ya kiufundi na kiutendaji na kuziwasilisha kwenye kamati ya Jumuiya na kwa Meneja wa RUWASA wa Wilaya

- (vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za mradi za Mwezi, Robo na na Mwaka na kuziwasilisha kwenye kamati ya Jumuiya na kwa Meneja wa RUWASA wa Wilaya
- (vii) Kusimamia matengenezo ya mradi na kutoa ushauri wa kiufundi kwa Meneja wa RUWASA wa Wilaya
- (viii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya mradi na\*-
- (ix) Kuhamasisha uchangiaji wa huduma ya maji, kutatua migogoro baina ya mteja /mwananchi na Jumuiya

## 2. MHASIBU WA JUMUIYA (NAFASI 1)

### SIFA ZA MUOMBAJI

- (viii) Awe na Cheti cha Kidato cha nne
- (ix) Awe na Cheti cha Uhasibu III na kuendelea
- (x) Awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa
- (xi) Awe na umri kuanzia miaka 18-35
- (xii) Awe na uzoefu wa kazi za Uhasibu usiopungua miaka miwili (2)
- (xiii) Awe na Ujuzi wa kutumia Kompyuta
- (xiv) Awe raia wa Tanzania
- (xv) Awe mwaminifu na mwadilifu na asiwe amewahi kufungwa jela

### MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa masuala ya fedha Jumuiya ya Watumiaji Maji katika Jumuiya ya Watumiaji Maji
- (ii) Kusimamia ukusanyaji wa malipo ya Ankara
- (iii) Kuandaa bajeti ya mwaka ya Jumuiya
- (iv) Kuandaa taarifa zote za fedha na kuziwasilisha kwa Msimamizi wa Jumuiya
- (v) Kufanya malipo baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Jumuiya na Meneja RUWASA Wilaya
- (vi) Kutunza Vitabu vya fedha, hati za Malipo na nyaraka zote za uthibitisho wa mopato na matumizi ya fedha
- (vii) Kupeleka fedha zote benki za makusanyoya Ankara za maji kabla ya matumizi
- (viii) Kushauriana na Msimamizi wa Jumuiya katika masuala yanayohusu fedha katika kutekeleza shughuli zote za mradi

## MSHAHARA

Kazi hii ni ya Mkatiba na Mshahara utalipwa kutokana na makusanyo ya mauzo

## VIAMBATANISHO

Maombi yote yaambatane na:-

- (i) Moelezo binafsi (CV)
- (ii) Vivuli vya Veti vya **Masomo** na **Mafunzo pamoja na Cheti cha kuzaliwa**


## NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Barua za maombi ziletwe kwa mkono katika Ofisi za RUWASA-Wilaya ya Lindi zilizopo Barabara ya Kawawa mkabala na makaburi ya Wahindi au yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

MENEJA WA RUWASA (W)  
S.L.P 430  
LINDI

**Maombi haya yatumwe kabla ya tarehe 19/01/2021 Saa 9:30 Alasiri.**

Tangazo hili limetolewa na;

KAMATI TENDAZI  
LINDI  
  
Ahmadi Abdallah Mtambo  
M/Kiti wa Jumuiya ya Watumiaji Maji  
RUTAMBA

05 Januari, 2020

6/1/2021